# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

**Mtaa wa Urambo,**

**Simu Nambari: 2150043 – 6/2150360**

**11102 ILALA**

**Fax No: (022) 2150047**

**ILALA – APRILI 11, 2019**

# TAARIFA KWA UMMA

## TAKUKURU MKOA WA ILALA YABURUZA MAHAKAMANI WATUHUMIWA 27 WA VITENDO VYA RUSHWA.

**NDUGU WANAHABARI.**

Ninapenda kuchukua fursa hii kuwashukuru sana kwa kuitikia wito wetu na kuja kushiriki kwenye mkutano huu. Karibuni sana ofisa za Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Ilala

**NDUGU WANAHABARI.**

Ni utaratibu wetu TAKUKURU kutoa taarifa ya utendaji kazi kwa umma katika kipindi cha kila robo mwaka kupitia kwenu wanahabari. Leo TAKUKURU Mkoa wa Ilala tunatoa taarifa ya utendaji kazi kwa kipindi cha Januari hadi Machi 2019. Kama inavyofafanuliwa hapa :

**i. MAHAKAMA**

Katika kipindi cha Januari hadi Machi 2019, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Ilala iliendelea na mashauri mahakamani yanahosu watuhumiwa 25, ambao wamejihusisha na vitendo vya rushwa. Miongoni mwa watuhumiwa hawa ni viongozi wa vyama vya siasa 3, Mtumishi wa Mahakama 1, Mtumishi wa Taasisi ya za Kifedha 1, watumishi wa sekta ya Elimu 3, watumishi wa TAMISEMI 5, watumishi wa Afya 5, na watumishi wa Sekta Binafsi 5, Mtumishi 1 wa Kampuni ya ujenzi.

**ii. UCHUNGUZI**

Katika kipindi hicho pia TAKUKURU Mkoa wa Ilala tumeendelea kufanya uchunguzi wa tuhuma mbalimbali kwa kufungua majalada ya uchunguzi 14, yanayohusu uhujumu uchumi, ukwepaji kodi, hongo, ubadhirifu wa mali ya umma, rushwa ya ngono, ujenzi wa miradi ya maendeleo chini ya kiwango. Uchunguzi wa majalada haya upo katika hatua mbalimbali.

**iii. UFUATILIAJI WA MIRADI YA MAENDELEO**

**Ndugu wanahabari**

Lengo la kufuatilia miradi ya maendeleo ni kuangalia thamani halisi ya fedha za umma kwenye ujenzi wa miradi hiyo. Ili kudhibiti uvujaji wa fedha za umma kwenye miradi ya maendeleo.

- Katika kipindi hiki tumefuatila miradi iliyoko katika Sekta za Afya, ujenzi wa Zahanati 2, Elimu, ujenzi wa madarasa 27 na matundu ya choo 10 kwenye shule 11, na Ujenzi wa Barabara 2. Miradi ya maji 3

  **Miradi yote iliyofuatiliwa ina thamani ya Shilingi 3,951,420,759.**

- Kati ya miradi hii 8 iliyokaguliwa TAKUKURU Mkoa wa Ilala imebaini miradi 4 ina viashiria vya rushwa. Uchunguzi tayari umeanzishwa ili kuwabaini watuhumiwa waliohusika na kuhujumu ujenzi wa miradi hii.

- Aidha katika kipindi hiki dawati limeshirikiana na Takukuru Makao Makuu katika kufuatilia miradi ya uboreshaji wa barabara tatu (3) ambazo ni Mpanda – Uvinza kwa kiwango cha lami kipande cha Mpanda – Kibo – Usimbili ( Mpanda – Ifukutwa – Vikonge ( 35Km) . Nyingine ni Uboreshaji wa barabara kwa kiwango cha lami Mbeya – Chunya - mkongolosi , kipande cha 3: Chunya – Makongolosi (39KM) na Ukarabati wa barabara vipande viwili vya njia kuu ya TANZAM Highway ) eneo la Iyovi hadi Kitonga na Ikokoto hadi Iringa ikijumuisha barabara ya Iringa (The Iringa access Road ), (149.Km)

**1. UELIMISHAJI UMMA.**

**1.1.** Kama nilivyotangulia kusema kuwa tunalo jukumu la Uelimishaji Umma. Katika kipindi cha Januari, 2019 – Machi, 2019,

Dawati la Elimu kwa umma Mkoa wa Ilala tumeweza kuelimisha makundi mbalimbali kwa njia ya semina ambapo semina 14 zimetolewa kwa makundi mbalimbali ambayo ni watumishi wa wakala wa vipimo, watumishi wa Tume ya ushindani, watumishi wa TRA, watumishi wa MOI, askari polisi wakaguzi na wapelelezi, watumishi wa TPDC, watumishi wa TANESCO, tumefungua klabu za wapinga rushwa katika shule za msingi 18, tumeimarisha klabu za

wapinga rushwa 6, tumefanya vipindi vya redio 5, mkutano 1 wa hadhara na onesho 1 la wiki ya sheria

*Katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2019, Tunatarajia kufungua na Kuimarisha Klabu za wapinga rushwa mashuleni na vyuoni, kuandaa vipindi redioni na Luninga pia kufanya mikutano ya hadhara.*

## 2. UTAFITI NA UDHIBITI

Katika kuhakikisha kuwa kero mbalimbali zinapatiwa ufumbuzi, na wakati mwingine kubaini mianya ya rushwa na hatimaye kupata njia sahihi ya kuishauri serikali kuhusiana na masuala ya rushwa katika mkoa wetu tumefanikiwa kufanya yafuatayo:

i. uchambuzi wa mfumo moja (3) , ikiwa ni katika matumizi ya risiti za EFD kwa wafanya biashara , Matumizi ya Nguvu kazi ya ndani katika kusimamia miradi ya ujenzi ( FORCE ACCOUNT) pamoja na ukusanyaji wa ushuru katika soko la samaki Feri.

*Tumejipanga kufanya ufuatiliaji wa miradi miwili ya Umma kwenye sekta ya maji na kufanya ufuatiliaji wa miradi mitatu ya ujenzi, iliyofuatiliwa siku za nyuma ambayo imeonesha mapungufu katika utekelezaji.*

**KUELEKEA UCHAGUZI**

**Ndugu wanahabari:**

Sote tunafahamu kuwa mwaka huu 2019 tutakuwa na Uchaguzi katika ngazi za Serikali za Mitaa na mwaka 2020 utakuwa ni Uchaguzi Mkuu, chaguzi hizi zinapaswa kuendeshwa na kusimamiwa kwa uadilifu na umakini mkubwa kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu ili haki, usawa, uhuru na demokrasia viweze kustawi, kuendelezwa na kudumishwa.

Rushwa katika Uchaguzi ni hatari na inaweza kuleta madhara kwa Taifa kwani viongozi wala rushwa au watoa rushwa hawataweza kuisimamia nchi kwa misingi ya haki, usawa, uwazi, uwajibikaji na uzalendo na vilevile wananchi wapokea au watoa rushwa hawawezi kuhoji masuala mbalimbali kwa viongozi wao.

Kwa kuzingatia umuhimu wa uchaguzi TAKUKURU tumejizatiti kufuatilia kwa umakini hatua kwa hatua uchaguzi huu, watakaojihusisha na vitendo vya rushwa hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

**MWISHO**

Ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa kukubali kuja kunisikiliza na hasa tukizingatia umuhimu wa shughuli yenu ya habari, napenda kutoa wito kwenu kuendelea kutoa elimu juu ya adui rushwa kwa jamii, na mwisho kabisa TAKUKURU inawaomba mkaendelee kuwa mabalozi madhubuti kwenye mapambano dhidi ya rushwa. Kalamu zenu zikawe silaha ya kuwaangamiza wala rushwa, tambueni kuwa ninyi ni wadau muhimu kwenye mapambano dhidi ya rushwa, anzisheni vipindi au makala maalum za kuingamiza rushwa kwenye vyombo vyenu.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA

**IMETOLEWA NA**
**Christopher Myava**
**KAMANDA WA TAKUKURU (M) ILALA**